

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



MKUTANO WA SABA

YATOKANAYO NA KIKAO CHA HAMSINI NA TATU

22 JUNI, 2017

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA HAMSINI NA TATU TAREHE 22 JUNI, 2017

I. DUA:

Saa 3:00 Mhe. Dkt. Tulia Ackson (Naibu Spika) alisoma Dua na kuongoza Kikao cha Bunge.

Makatibu mezani:

1. Ndg. Theonest Ruhilabake
2. Ndg. Joshua Chamwela

II. MASWALI

OFISI YA WAZIRI MKUU

Swali Na. 437: Mhe. Ussi Salum Pondeza (liliulizwa na Mhe. Dkt. Faustine Ndugulile)

Nyongeza: Mhe. Ussi Salum Pondeza
Mhe. Joseph Roman Selasini

OFISI YA RAIS (TAMISEMI)

Swali Na. 438: Mhe. Mussa Ramadhani Sima

Nyongeza: Mhe. Mussa Ramadhani Sima
Mhe. Mussa Rashid Ntimizi
Mhe. Riziki Shahari Mngwali
Mhe. Mary Pius Chatanda
Mhe. Oran Manase Njeza

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII

Swali Na. 439: Mhe. Vedasto Edgar Ngombale (liliulizwa na Mhe. Zubeir Mohamed Kuchauka)

Nyongeza: Mhe. Vedasto Edgar Ngombale
Mhe. Edwin Mgante Sannda
Mhe. Anthony Calist Komu
Mhe. Mchg. Peter Simon Msigwa
Mhe. Dkt. Dalali Peter Kafumu
Mhe. Sixtus Raphael Mapunda

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA

Swali Na. 450: Mhe. Susan Limbweni Kiwanga

Nyongeza: Mhe. Susan Limbweni Kiwanga
Mhe. Issa Ali Mangungu
Mhe. Joram Ismael Hongoli
Mhe. Susan Anselm Lyimo
Mhe. Pauline Philipo Gekul

III. MATANGAZO

- (i) Wageni mbalimbali waliokuwepo Bungeni walitambulishwa.
- (ii) Wajumbe wa Kamati ya Uongozi watakuwa na Kikao leo Ukumbi wa Spika.

MIONGOZO:

1. Mhe. Mchg. Peter Simon Msigwa aliomba Mwongozo wa Spika kwa Kanuni ya 47 na kuomba Bunge liahirishwe ili kujadili jambo la dharua linalohusu mauaji ya Raia na Askari Polisi yanayotokea huko Kibiti/Rufiji.

Naibu Spika alieleza kuwa Kanuni ya 47 inapaswa kusomwa pamoja na Kanuni ya 48 na kwa mujibu wa Kanuni 47(4) ni wazi kwamba jambo hilo linashughulikiwa na Serikali hivyo haitakuwa mwafaka kujadiliwa na Bunge.

2. Mhe. Goodluck Asaph Mlinga aliomba Mwongozo wa Spika na kuuliza kwa nini Kituo Kikuu cha Polisi Mkoani Dodoma hakina umeme kwa muda mrefu sasa.

Naibu Spika alieleza kuwa Kiti hakina uwezo wa kutoa Mwongozo kwenye jambo hilo kwa kuwa halijatokea Bungeni.

IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

- (i) Waziri wa Fedha na Mipango aliwasilisha Maelezo ya Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka, 2017 (*The Finance Bill 2017*) na kutoa Hoja kwamba Muswada huo sasa usomwe kwa Mara ya Pili na kujadiliwa na Bunge.
- (ii) Mwenyekitia wa Kamati ya Bajeti, Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia aliwasilisha Taarifa ya Kamati yake kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka, 2017.
- (iii) Msemaji wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Fedha na Mipango, Mhe. David Ernest Silinde aliwasilisha Maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka, 2017.

MJADALA WA JUMLA

Mjadala wa Jumla wa Wabunge ulianza kama ifuatavyo:-

- | | |
|---|---------|
| 1. Mhe. Dkt. Balozi Diodorus Buberwa Kamala - | CCM |
| 2. Mhe. Japhet Ngailonga Hasunga - | CCM |
| 3. Mhe. Dkt. Mary Machcha Mwanjelwa - | CCM |
| 4. Mhe. Hussein Mohamed Bashe - | CCM |
| 5. Mhe. Pauline Philipo Gekul - | CHADEMA |
| 6. Mhe. Riziki Said Lulida - | CUF |

7. Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia - CCM

Kiti kilitoa ufafanuzi kuhusu Wabunge kuomba miongozo kuhusiana na ubaguzi.

(V) KUSITISHA BUNGE

Saa 7:00 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 10:00 jioni.

(VI) BUNGE KUREJEA

Saa 10:00 jioni Bunge lilirejea, Mjadala wa Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2017 uliendelea kwa Wabunge wafuatao kuchangia:

- | | | |
|--|---|---------|
| 8. Mhe. Jitu Vrajlal Soni | - | CCM |
| 9. Mhe. Selemani Jumanne Zedi | - | CCM |
| 10. Mhe. Pascal Yohana Haonga | - | CHADEMA |
| 11. Japhary Raphael Michael | - | CHADEMA |
| 12. Mhe. Josephat Sinkamba Kandege | - | CCM |
| 13. Mhe. Richard Philip Mbogo | - | CCM |
| 14. Mhe. Prof. Anna Kajumulo Tibaijuka | - | CCM |
| 15. Mhe. Munde Tambwe Abdallah | - | CCM |
| 16. Mhe. George Mchechu Masaju | - | AG |

Mtoa hoja, Waziri wa Fedha na Mipango alihitimisha Hoja yake kwa kujibu michango iliyotolewa na Wabunge na kutoa Hoja.

VII. KAMATI YA BUNGE ZIMA

Bunge liliingia katika hatua ya Kamati ya Bunge Zima ili kupitisha Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka, 2017 Ibara kwa Ibara. Mhe. Japhary Raphael Michael na Mhe. Ruth Hiyob Mollel waliwasilisha mapendekezo ya kufanya marekebisho ambayo hayakukubaliwa. Bunge lilipitisha Muswada huo pamoja na marekebisho ya Serikali.

VIII. TAARIFA

Mtoa Hoja alitoa Taarifa ya Kazi ya Kamati na kutoa Hoja, Bunge lilihojiwa na kupitisha Muswada huo.

IX. KUSOMWA MARA YA TATU

Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka, 2017 ulisomwa Mara ya Tatu na hivyo kupitishwa na Bunge.

X. KUAHIRISHA BUNGE

Saa 12:40 jioni Bunge liliahirishwa mpaka kesho Ijumaa tarehe 23 Juni, 2017 saa 3:00 asubuhi.